# Mustakabali wa Ufundishaji na Ujifunzaji wa Fonolojia ya Kiswahili kwa kutumia Uwili Lugha katika Elimu ya Juu Tanzania: Mifano kutoka Programu za Uzamili

Joseph Hokororo Ismail, Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto, P.O. Box 20, LUSHOTO-TANZANIA

na

Baraka Kasinge Mwikwabe, Chuo Kikuu cha Mt. Agustino, Bewa Kuu Mwanza, P. O. Box 307, MWANZA, TANZANIA

***Ikisiri***

Tangu serikali ipanue wigo wa utoaji elimu ya juu Tanzania, hususani elimu ya Chuo Kikuu, kumekuwa na ongezeko la vyuo vikuu vinavyotoa elimu ya Juu. Ongezeko hili limechangiwa na taasisi zisizo za umma kuanzisha vyuo vikuu binafsi ambavyo hutoa shahada kuanzia za awali mpaka za Uzamivu kwa kutumia ama lugha ya Kiswahili au Kiingereza. Katika vyuo Vikuu hivi, lugha ya Kiswahili imekuwa ikitumika kujifunzia na kufundishia somo la Kiswahili na taaluma za Kiswahili kwa shahada za awali. Katika jitihada za kupanua taaluma za Kiswahili, baadhi ya vyuo vikuu hapa Tanzania, kama vile Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Chuo Kikuu cha Ruaha na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, vinafundisha taaluma za Kiswahili kwa lugha ya Kiswahili katika kiwango cha shahada ya Uzamili na Uzamivu. Hivyo, kozi za fasihi na isimu kama vile fonolojia, mofolojia, semantiki, sintaksia, isimu Jamii, kuyataja kwa uchache, katika ngazi za uzamili hufundishwa kwa lugha ya Kiswahili. Katika ufundishaji na ujifunzaji wa taaluma za Kiswahili kwa kutumia lugha ya Kiswahili kumekuwa na changamoto za namna Kiswahili inavyowezesha ufundishaji na ujifunzaji wa fonolojia katika ngazi ya Umahiri na Uzamivu. Lengo la makala haya ni kujadili mustakabali wa ufundishaji wa fonolojia katika ngazi ya Umahiri kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Vyuo vikuu viwili vilitumika kama sampuli ya kukusanya data na Mkabala wa Kifafanuzi na Ulinganisho zilitumika katika uchambuzi wa data. Utafiti huu utasaidia kuona aina ya maboresho yanavyoweza kufanyika hasa katika kipengele cha tafsiri za istilahi za fonolojia yanayoweza kusaidia kukuza taaluma ya fonolojia na lugha ya Kiswahili kwa ujumla kwa kuwa vitabu mbalimbali vya fonolojia (vingi) vimeandikwa kwa lugha ya Kiingereza ambayo huwatatiza wajifunzaji na wafundishaji. Makala yanahitimisha kwamba pamoja na changamoto za tafsiri na ukosefu wa vitabu vya rejea vilivyoandikwa kwa lugha ya Kiswahili, upo mwanga mkubwa kwamba lugha ya Kiswahili inaweza kutoa maarifa ya kutosha kuhusu taaluma ya fonolojia kwa ujumla wake.

**Dhana za Msingi:** Kiswahili, fonolojia, ufundishaji, ujifunzaji, elimu ya juu.

## UTANGULIZI

Makala haya yalilenga kujadili mustakabali wa ufundishaji na ujifunzaji wa fonolojia ya Kiswahili kwa kutumia uwili lugha katika elimu ya juu Tanzania hususani programu za Uzamili. Kama inavyoonekana katika sehemu ya ikisiri, utafiti huu umehusisha vyuo vikuu viwili vya umma vinavyofundisha kozi ya fonolojia ya Kiswahili katika kiwango cha Umahiri. Kihistoria, katika miaka ya 2000, kumekuwa na mwamko na mjadala mkubwa wa taasisi za elimu hapa Tanzania kuona uwezekano wa kutumia lugha ya Kiswahili kama chombo cha kufundishia na kujifunzia masomo mbalimbali katika ngazi zote za elimu ya juu. Hali ya mijadala hii ilipelekea kuwa na matamko yaliyotilia maanani utekelezaji ama kuunga mkono kwa hoja ya kukifanya Kiswahili kuwa lugha ya kufundishia na kujifunzia, kwa mfano vikao mbalimbali vya Mabaraza ya Uongozi wa Vyuo Vikuu kuendeshwa na kuchukuliwa mihtasari ya vikao hivyo kwa Kiswahili. Aidha baadhi ya taasisi kama vile Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, zimeanzisha programu za Kiswahili katika ngazi za shahada ya awali mpaka shahada ya Uzamivu. Tunapozungumzia shahada za awali tunamaanisha shahada ya kwanza, shahada ya Umahiri inamaanisha shahada ya Pili na shahada ya Uzamivu inamaanisha shahada ya Udaktari wa Falsafa. Hivyo kwa mujibu wa programu za Kiswahili, kunakuwa na Shahada ya Awali (Kiswahili); Shahada ya Umahiri (Kiswahili) na Shahada ya Uzamivu (Kiswahili),

Hapa Tanzania, kupitia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kulikuwa na programu ya Umahiri ambayo hapo awali imekuwa ikifundishwa kwa ushirikiano baina ya idara ya Kiswahili na idara ya lugha za kigeni na isimu. Wafanyakazi ,wanataaluma na wasio wanataaluma wamepata mafunzo kupitia programu hii. Hata hivyo, kwa sababu ya muundo wa programu yenyewe, Kiswahili kama somo, hakikuzingatiwa ipasavyo. Taaluma za Kiswahili kama vile isimu na matawi yake, Fasihi na matawi yake na Uchapishaji na mawasiliano havikuzingatiwa. Kutokana na mapungufu haya, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ikaamua kuanzisha programu ya ufundishaji wa Taaluma za Kiswahili, ikiwemo fonolojia ya Kiswahili.

Malengo Makuu ya Programu ya MA (Kiswahili) yameainishwa katika Silabasi ya Programu ya MA Kiswahili (2010) kama ifuatavyo:

a) Kuandaaa wataalamu ambao watafundisha taaluma za Kiswahili kwenye ngazi za elimu ya juu;

b) Kuandaa wataalamu watakaofanya kazi katika vyombo vya habari, mashirika ya uchapishaji, idara za serikali, mashirika ya Kimataifa na maeneo mengineyo husika;

c) Kufunza wanafunzi watakaoweza kusoma masomo ya Uzamivu katika isimu na /au fasihi ya Kiswahili.

Kutokana na malengo haya, lugha ya kufundishia na kuandikia tasnifu ni Kiswahili.

Baada ya kuangalia usuli unaohusu ufundishaji wa programu ya Umahiri kwa ujumla, sasa tuangalie kwa ufupi kuhusu programu ya kozi ya fonolojia katika Umahiri. Madhumuni ya msingi ya kozi hii ni kuwawezesha wanafunzi kuzielewa nadharia za sasa za viwango vya juu vya fonolojia na jinsi nadharia hizo zinavyoweza kutumika katika kuvichambua na kuvichanganua vipengele mbalimbali vya fonolojia ya Kiswahili. Kozi inaanza kwa kupitia maoni mbalimbali yaliyotolewa dhidi ya Modeli Rasmi (MR) ya mkabala wa Fonolojia Zalishi (FZ). Kisha itaelezea baadhi ya nadharia na mikabala iliyopendekezwa ili kuepukana na matatizo yaliyojitokeza katika Kiunzi Msingi hicho. Katika kufundisha nadharia hizi kozi itakuwa ikifanya ulinganisho baina ya Kiswahili na lugha nyingine za kibantu. Kutokana na usuli huu,

Katika kufundisha programu ya fonolojia ya Kiswahili, ilitarajiwa kwamba lugha ya kufundishia na kujifunzia programu hii iwe Kiswahili, kwamba mhadhiri aitumie lugha ya Kiswahili katika ufundishaji wa Kiswahili kwa ufasaha na michango na majadiliano ya wanafunzi darasani, na Makala mbalimbali yanayoandikwa na wanafunzi kwa minajili ya kukidhi tathimini za programu ziandikwe kwa Kiswahili sanifu na fasaha. Hivyo, makala haya yanaangazia kujadili mustakabali wa ufundishaji na ujifunzaji wa fonolojia ya Kiswahili kwa kutumia lugha ya Kiswahili kama lugha ya kufundishia na kujifunzia. Malengo mahususi yatakuwa Kujadili namna ambavyo lugha ya Kiswahili na Kiingereza zinavyotumika katika ufundishaji na ujifunzaji wa fonolojia ya Kiswahili darasani; Kuangalia matumizi ya Kiswahili katika kuandika kazi na vitabu vya fonolojia ya Kiswahili na Kutathimini ujitoshelezaji wa vitabu vya rejea vilivyoandikwa kwa Kiswahili kuhusu fonolojia ya Kiswahili. Utafiti huu umeongozwa na maswali yafuatayo:

a) Je lugha ya Kiswahili na Kiingereza zinatumikaje katika ufundishaji na ujifunzaji wa fonolojia ya Kiswahili darasani?

b) Je vitabu na kazi za wanafunzi za fonolojia ya Kiswahili zimeandikwa kwa Kiswahili fasaha? na

c) Je kuna vitabu vya kutosha vilivyoandikwa kwa Kiswahili kuhusu fonolojia ya Kiswahili?

Utafiti huu utatoa mchango mkubwa katika fonolojia ya Kiswahili kwa kuwa utapendekeza mikakati stahiki ya kukabiliana na changamoto zitakazoonekana kujitokeza katika ufundishaji na ujifunzaji wa fonolojia ya Kiswahili. Aidha utachangia katika kuhamasisha wataalamu wa fonolojia na taaluma ya isimu kwa ujumla namna ya kujipanga kwa kufanya uchunguzi wa kutosha na kutoa machapisho ya kutosha kuhusu taaluma ya fonolojia ya Kiswahili kwa lugha ya Kiswahili. Hivyo kupunguza changamoto za ufundishaji na ujifunzaji wa fonolojia ya Kiswahili kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Baada ya kuangalia usuli wa tatizo letu la utafiti, tuendeleze mjadala huu kwa kuangazia wataalamu kadhaa walioandika kuhusu ufundishaji wa lugha na dhana ya uwili lugha, tukianza na Brown na Atkins hapa chini.

Brown na Atkins (1988) wanafafanua mchakato wa ufundishaji kama utoaji wa fursa za kujifunza kwa wanafunzi. Kujifunza ni mchakato wa kupata mafunzo yanayokusudiwa kwa mwanafunzi au mtu anayejifunza. Brown na Atkins wanaongeza kwa kusema kuwa mchakato wa kufundisha na kujifunza ni wa mwingiliano na ni zoezi lenye makusudio fulani. Mambo yanayotakiwa kufunzwa kwa wanafunzi inaweza kuwa uhalisia, michakato, ujuzi, mawazo (dhana), na mitazamo. Hata hivyo, inasisitizwa kuwa wanafunzi, si wakati wote, watajifunza kile tunacholenga wajifunze, wakati mwingine wanaweza kujifunza dhana ambazo hatukukusudia wao kujifunza.

Lisilo budi ni kwamba, mchakato wa kufundisha na kujifunza hutegemea lugha. Mara nyingi lugha ya kufundishia na kujifunzia huelekezwa na sera ya elimu au sera ya lugha ya jamii husika. Kwa Tanzania, hususani kwa elimu ya juu ambayo ndio lengo la utafiti huu, Sera Mpya ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 inaelekeza kwamba lugha ya Taifa ya Kiswahili itatumika kufundishia na kujifunzia katika ngazi zote za elimu na mafunzo na Serikali itaweka utaratibu wa kuwezesha matumizi ya lugha hii kuwa endelevu na yenye ufanisi katika kuwapatia walengwa elimu na mafunzo yenye tija kitaifa na kimataifa. Sera hiyo inaongeza kuwa serikali itaendelea na utaratibu wa kuimarisha matumizi ya lugha ya Kiingereza katika kufundishia na kujifunzia, katika ngazi zote za elimu na mafunzo (JMT, 2014).

Hata hivyo, kuutokana na sababu mbalimbali, katika vyuo vikuu kumekuwepo na mazoea ya uwili lugha ambapo badala ya lugha ya kufundishia kutumika kama lugha pekee, walimu na wanafunzi hujikuta wakitumia lugha zaidi ya moja. Dhana hii ya uwili lugha, ni dhana inayoweza kuleta utata inaposikika kwa wazungumzaji wa Kiswahili, kadhalika kwa msomaji wa kazi hii. Tafsiri ya kwanza, mtu anaweza kujiuliza kama uwili lugha ni matumizi ya lugha mbili kama mfumo rasmi wa jamii?[1] Au ni matumizi ya lugha mbili katika mazungumzo iwe ni kuchanganya katika sentensi au kuongea kwa lugha moja kisha mzungumzaji akahamia kwenye lugha nyingine lakini akiendelea na mazungumzo yale yale?[2] Vyovyote iwavyo, kwa kuwa lengo letu si kueleza ufanano wala tofauti za dhana hizo katika Kiswahili, katika makala haya tutatumia neno *uwili lugha* kama matumizi ya lugha zaidi ya moja katika ufundishaji na ujifunzaji bila kujali ni mfumo-lugha ulio rasmi au si rasmi. Kwa maneno mengine, katika utafiti huu, neno uwili lugha linatumika kwa kuzijumuisha dhana mbili za Kiingereza "Bilingualism" na "Code switching/code mixing".

Katika muktadha wa elimu, uwili lugha unaweza kuwa ni mfumo wa kitaasisi au wa watu binafsi. Kama anavyofafanua Du Plessis (2006), uwili lugha wa kitaasisi ni mfumo lugha wa taasisi husika kutumia lugha mbili hata kama hazitumiki katika ufundishaji na ujifunzaji. Aina hii ya uwili lugha, pia, inafafanuliwa na Langner & Imbach (2000) kama matumizi ya lugha mbili katika shughuli za taasisi fulani. Ilhali uwili lugha wa watu binafsi ni matokeo ya taasisi

[1] "Bilingualism"

[2] "Code switching/code mixing"

inayotumia au kutambua matumizi ya lugha mbili (Du Plessis, 2006). Kutokana na hali au mfumo huo wa lugha, uwili lugha kwa watu binafsi ni matokeo ya kiisimujamii ya mfumo-lugha wa taasisi (chuo, kwa muktadha huu) ambapo washiriki[3] wa chuo husika hutumia lugha zaidi ya moja. Utafiti huu unajikita katika mfumo wa uwili lugha darasani. Lin (2013) anafafanua matumizi ya uwili lugha darasani kama utumiaji wa lugha zaidi ya moja darasani miongoni mwa washiriki wa darasa (walimu na wanafunzi).

Ni ukweli usiopingika kuwa ufundishaji wa kozi za fasihi na isimu kama vile fonolojia, mofolojia, semantiki, sintaksia, isimujamii, kwa uchache, katika ngazi za uzamili kwa lugha ya Kiswahili unakabiliwa na changamoto kadhaa. Kwa kujikita katika fonolojia, kama kipengele mahsusi cha utafiti huu, walimu wa fonolojia wanakumbana na fonolojia wanakumbana na changamoto kama vile ugumu katika kueleweka kwa istilahi za fonolojia pamoja na uhaba wa dhana za kifonolojia katika vitabu mbalimbali vilivyoandikwa kwa Kiswahili. Ili kukabiliana na tatizo, baadhi ya wakufunzi hulazimika kutumia mbinu mbalimbali ikiwemo mbinu ya uwili lugha. Ni kutokana na changamoto hii, utafiti huu ulilenga kuchunguza na kujadili changamoto na mustakabali wa namna ufundishaji wa fonolojia katika ngazi ya Umahiri kwa kutumia lugha ya Kiswahili.

## MAPITIO YA MAANDIKO JARABATI

Watafiti walihusisha mapitio tangulizi kadha wa kadha ili kupata ufahamu wa kutosha juu ya mada hii. Katika sehemu hii, baadhi ya mapitio yanayohusu uwili lugha yameelezwa kwa ufupi kama ifuatavyo.

### a) Sababu na Malengo ya Utumiaji wa Uwili Lugha katika Ufundishaji na Ujifunzaji

Sababu au malengo ya uwili lugha katika ufundishaji yameelezwa na wataalamu mbalimbali ambao wanaelekea kufanana kwa sababu zilizo nyingi. Sababu na malengo hayo ni kama ifuatavyo.

Sababu mojawapo ni kusisitiza dhana kwa kuirudia; hii ni pale ambapo mwalimu huamua kueleza dhana fulani kwa lugha zote mbili ili ieleweke zaidi (Lewis, 2008; Shartiely, 2016; Flyman-Mattsson and Burenhult, 1999). Sababu nyingine ni malengo ya kumudu darasa (Shartiely, 2016; Flyman-Mattsson na Burenhult, 1999). Pia, kuhamisha mada ya mazungumzo (Flyman-Mattsson na Burenhult, 1999; Shartiely, 2016). Sababu nyingine ni walimu kuonesha umoja na mshikamano kwa wanafunzi wao (Merritt na wenzake, 1999; Flyman-Mattsson and Burenhult, 1999). Lengo lingine ni kuonesha hisia katika uelekezaji (Flyman-Mattsson and Burenhult, 1999).

Wengine wanadai walimu hutumia uwili lugha kwa kukosa msamiati wa lugha moja kueleza dhana fulani (Flyman-Mattsson and Burenhult, 1999; Merritt na wenzake, 1992; Shartiely,

[3] Wahadhiri, wanafunzi na wafanyakazi wengine wa taasisi husika.

2016). Nao Shartiely (2016) na Blommaert (2008) wanadai uwili lugha hutumika ili mzungumzaji aweze kueleweka vema. Naye Skiba (1997) anaongeza kuwa kuwa uwili lugha husaidia wazungumzaji kuwasilisha ujumbe wao kama inavyotakiwa. Wengine ni García na Wei (2014), wao wanasema uwili lugha huwasaidia wanafunzi wa jamii zenye uwingi-lugha kuendanisha dhana wanazojifunza na uzoefu[4] wao.

Ni kutokana na sababu hizo, wataalamu kama Rugemalira (2017), moja ya mapendekezo yake, ni kuboresha mfumo wa uwili-lugha katika elimu ya vyuo vikuu ambapo anapendekeza lugha ya Kiswahili iruhusiwe kutumika walau kwa matumizi ya rasha rasha hususani katika mihadhara, semina, majadiliano pamoja na mitihani.

**b) Mambo ya Kuzingatia katika Utumiaji wa Uwili Lugha katika Ufundishaji na Ujifunzaji**

Hata hivyo, licha ya uwepo wa sababu za msingi za uwili lugha katika ufundishaji, baadhi ya wataalamu wanashauri kuwepo kwa umakini katika mfumo huu. Kwa upande wake, Brisk (2000) anadai kuwa uthabiti wa uwili lugha hutegemeana na mambo muhimu katika kozi husika kama vile mafunzo aliyoyapata mwalimu, mtaala, nyenzo zitumikazo, uwasilishaji wa mwalimu darasani, na mbinu zitumikazo katika tathmini ya upimaji. Nao Madrid na Julius (2017) wanasisitiza kuwa mafanikio ya ufundishaji kwa uwili lugha hupimwa kwa matokeo kwa wanafunzi ikiwemo umilisi wa lugha, maendeleo ya kitaaluma, na mtagusano wa kijamii na kiutamaduni. Wanaongeza kwamba mafanikio ya uwili lugha hutegemea tambia za wanafunzi pamoja na familia.

Nao Villareal na Solís (1998) wanaripoti juu ya sababu zinazochangia kufanikiwa kwa ufundishaji kwa uwili lugha ambapo wanabainisha vitu kadhaa, vifuatavyo ni baadhi ya vitu hivyo: malengo bayana, watekelezaji wenye uelewa unaotakikana, uwezeshaji wa mamlaka zinazosimamia mfumo wa elimu, maelekezo toshelevu kwa kozi husika, njia mwafaka za upimaji wa wanafunzi, vifaa toshelezi na vyenye kuendana na uwili-lugha, uwasilishaji wa somo uwe shirikishi, collaborative, meaningful, na unaojali na kujibu mahitaji binafsi ya wanafunzi mmoja mmoja.

Kwa ujumla, Madrid na Julius (2017) wanadai kuwa tafiti nyingi zinaonesha kwamba uthabiti wa ufundishaji kwa kutumia uwili lugha unaweza kutazamwa kwa vigezo mbalimbali ikiwemo wanafunzi wenyewe, jamii, shule, mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji darasani, aina ya somo/kozi inayotolewa, miktadha mbalimbali kama vile wa kijamii, kisiasa na utamaduni, pamoja na matokeo yanayopatikana. Wanaongeza kuwa kufanikiwa kwa ufundishaji wa uwili lugha hutegemea uhusiano mzuri wa vigezo tajwa hapo juu.

[4] Mambo ambayo tayari mtu anayafahamu kutokana na pilikapilika za kimaisha

**c) Tafiti Juu ya Utumiaji wa Uwili Lugha katika Ufundishaji na Ujifunzaji**

Tukitazama upande wa kiwango cha matumizi ya uwili lugha katika ufundishaji na ujifunzaji darasani, kuna tafiti mbalimbali zilizokwisha kufanyika. Zifuatazo ni baadhi tu ya tafiti hizo.

Katika utafiti wake katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Shartiely (2016) alibaini kwamba wakufunzi walitumia uwili lugha kwa kuchanganya Kiswahili na Kiingereza zenye ili kuchangamana na wanafunzi, kuhawilisha dhana fulani, kufafanua jambo, kumudu darasa ama/na kushauri au kuhamasisha wanafunzi wao. Utafiti wake ulibaini kuwa uwili lugha katika chuo hicho hutokea katika namna mbili, mojawapo ni pale ambapo wakufunzi wa chuo hicho wanapotumia Kiswahili na Kiingereza kulingana na muktadha kutokana na sababu kwamba chuo hicho kinajumuisha wafanyakazi wa wanataaluma na wasiowa wanataaluma. Namna nyingine ni kwamba Kiswahili na Kiingereza hutumika darasani hususani katika mihadhara ambapo Kiswahili na Kiingereza hutumika kwa lengo la kukidhi mahitaji ya kimawasiliano. Mtafiti huyo anakazia kwamba wahadhiri wote nane walioshiriki katika utafiti huo hutumia uwili lugha na hili halijitokezi kwa bahati mbaya bali wanakusudia kwa sababu mbalimbali kama ilivyodhihirika katika sehemu (a) huko juu.

Ibrahim na wenzake (2013) wanaripoti kwamba walimu wafundishao lugha hutumia uwili lugha darasani ingawa wao walikataa kwamba hawatumii. Katika uchunguzi wao walibaini kwamba mara nyingi uwili lugha hutumika kwa malengo ya mbinu za kiufundishaji.

Nao Bhatti na wenzake (2018) katika utafiti wao walibaini kuwa uwili lugha hutumika darasani ingawa Kiingereza hubaki kama lugha kuu ya kufundishia katika vipindi husika. Kwa mujibu wao, wahadhiri huchanganya lugha kwa kukusudia. Wanahitimisha kwa kusema kuwa uwili lugha ni mbinu mwafaka katika ufundishaji wa lugha kwa kuwa huwezesha zaidi ufundishaji na ujifunzaji. Mtazamo huu ni sawa na Songxaba na wenzake (2017) wanaodai kuwa washiriki wa utafiti wao walionesha mtazamo chanya juu ya matumizi ya uwili lugha na kwamba hurahisisha uelewa. Songxaba na wenzake wanaenda mbali zaidi kwa kupendekeza mbinu hii itambulike kama mfumo rasmi katika ngazi zote.

Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Marie (2013) nchini Rwanda, Uwili lugha ni moja ya mbinu ambazo wanafunzi wa vyuo vikuu, nchini humo, huzitumia kukabiliana na changamoto zitokanazo na matumizi ya Kiingereza kama lugha ya kufundishia na kujifunzia. Utafiti huo ulibaini kuwa wanafunzi hao hutumia Kinyarwanda katika kujifunza Kiingereza kwa kuwa Kinyarwanda ndio lugha mama inayowaunganisha wote. Hata hivyo, ilibainika kwamba dhana za msingi hubaki kwa Kiingereza kutokana na kukosekana kwa msamiati wa Kinyarwanda unaolingana na dhana hizo. Utafiti unapendekeza kwamba japokuwa Kinyarwanda hakitambuliki kama lugha rasmi ya kufundishia, si budi kizingatiwe kwa kuruhusu uwili lugha wakati wa mihadhara darasani au katika vikundi vya wanafunzi.

Makulloluwa (2013) anadai kuwa, katika utafiti wake, washiriki wengi walionesha kupendezwa na matumizi ya uwili lugha katika ufundishaji wa lugha ya pili kwa sababu kwamba mbinu hiyo, kupitia lugha ya kwanza, hurahisisha ufahamu kwa lugha ya pili. Makulloluwa anapendekeza kwamba walimu wanatakiwa kupewa mafunzo zaidi juu ya ufaafu wa lugha ya kwanza katika ujifunzaji wa lugha ya pili.

Tofauti na watafiti wengine, kwa upande wake, Johanes (2017) anauona mtindo huu (uwili lugha) kuwa unarudisha nyumba ufundishaji na ujifunzaji wa lugha. Katika utafiti wake alibaini kuwa uwili lugha darasani hupelekea wanafunzi kutofanikiwa katika kujifunza Kiingereza kwa sababu hupelekea wanafunzi kushindwa kujiamini wanapoongea, huwanyima wanafunzi fursa ya wanafunzi kujaribu kuzungumza Kiingereza. Johanes anaongeza kuwa walimu ndio chanzo kikuu cha tabia hii na kwamba juhudi zaidi zinahitajika kwa walimu ili kuboresha uwezo wao wa kimethodolojia.

**Pengo la Utafiti**

Kutokana na mapitio yote hapo juu, wengi kati ya wataalamu wote wanajadili uwili lugha kwa kujikita katika upande wa majukumu ya mawasiliano nje au darasani. Hata wale wanaojadili kuhusu suala hili katika vipindi vya somo la Kiingereza bado wanazitazama faida na hasara za uwili lugha katika kona ya uwezeshaji wa mawasiliano tu. Mjadala wao haujikiti sana katika faida au hasara za uwili lugha katika upataji maarifa kwa kujikita katika nyanja, somo au mada mahsusi. Upungufu huu wa data zilizopo ndio uliowapelekea waandishi wa makala haya kulenga kujadili changamoto na mustakabali wa namna ufundishaji wa fonolojia katika ngazi ya uzamili kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu data zilizopo si sahihi kuzitumia kuhitimisha juu ya faida na hasara za uwili lugha katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuwa changamoto za ufundishaji wa lugha hasa isimu hutofautiana kulingana na viwango vya kiisimu.

## MBINU ZA UTAFITI

Kwa kuwa lengo la makala haya ilikuwa ni kujadili mustakabali wa ufundishaji na ujifunzaji wa fonolojia ya Kiswahili katika ngazi ya Umahiri kwa kutumia lugha ya Kiswahili, watafiti walichagua vyuo viwili vilivyotumika kama sampuli ya kukusanya data, Vigezo vya kuchagua vyuo hivi ilikuwa kama vyuo husika vinafundisha kozi ya fonolojia ya Kiswahili kwa kutumia lugha ya Kiswahili katika kiwango cha Umahiri. Ili kuzingatia maadili ya kiutafiti, vyuo hivi tumevipa majina dhahania (majina yasiyo halisi) ya Chuo Kikuu A na Chuo Kikuu B. Izingatiwe kwamba Majina A na B haihusiani na tafsiri kwamba Chuo kilichoitwa jina la chuo A ni bora kuliko kile kilichoitwa Chuo B.

Walengwa wakuu katika utafiti huu walikuwa ni wahadhiri wa somo la fonolojia ya Kiswahili pamoja na wanafunzi wa uzamili waliokuwa wanasomea fonolojia ya Kiswahili. Vyuo vilichaguliwa kwa kutumia mbinu ya kusudio na baadhi ya vigezo vilikuwa ni uwepo wa programu ya uzamili hususani Isimu kwa Kiswahili na utolewaji wa kozi ya fonolojia katika chuo husika. Pia, walimu na wanafunzi waliolengwa ni wale waliokuwa wanafundisha na

kusomea fonolojia ya Kiswahili (mtawalia). Wahusika kwa chuo A, darasa la fonolojia lilikuwa na wanafunzi 20, hivyo wanafunzi wote 20 walishiriki katika mahojiano walisampulishwa kwa kutumia mbinu ya kusudio-rahisi ambapo walipatikana kwa kadri watafiti walivyokutana nao au walivyokuwa tayari kwa majadiliano. Pia katika Chuo B, darasa la fonolojia ya Kiswahili lilikuwa na wanafunzi 15 ambapo pia wote walishiriki katika mahojiano ya utafiti huu. Ili kupima ulinganifu, utafiti ulihusisha wahadhiri na wanafunzi wa isimu katika programu za uzamili (Kiswahili).

Data za utafiti huu zilipatikana kwa kutumia mbinu zifuatazo:

**Mbinu ya mahojiano**: Mbinu ya mahojiano ilitumika kupata mawazo na mitazamo ya walimu na wanafunzi juu ya mustakabali wa ufundishaji na ujifunzaji wa fonolojia ya Kiswahili kwa kutumia uwili lugha katika vyuo vyao na mfumo wa elimu ya juu Tanzania kwa ujumla. Kwa upande wa mbinu ya mahojiano, wanafunzi na walimu walihojiwa kwa nyakati tofauti katika maongezi ya kawaida yahusuyo masomo. Hii ilikuwa ni mbinu faafu kwa sababu wahusika walijieleza vema na kuonesha mitazamo yao halisi kuliko wangekuwa wanajua kuwa wanahojiwa kwa ajili ya utafiti. Lengo la kutokuwataarifu ilikuwa ni kupata data halisi.

**Njia ya Ukusanyaji Data Maktabani na Makavazini:** Kulikuwa na usomaji wa muhistasari wa kozi ya fonolojia kwa vyuo vyote viwili na vitabu vya fonolojia vilivyoandikwa kwa Kiswahili. Kwa kutumia njia hii, mtafiti aliweza kuona idadi ya vitabu vya fonolojia vilivyoandikwa kwa Kiswahili kulinganisha na vile vilivyoandikwa kwa Kiingereza, pia, kwa vitabu vile vilivyoandikwa kwa lugha ya Kiswahili, mtafiti alisoma vitabu vyote kuona kama vimeandikwa kwa lugha ya Kiswahili ama kulikuwa na mchanganyiko wa lugha iliyotumika na Kiingereza au lugha nyingineyo. Baadhi ya vitabu ambavyo mtafiti alivisoma kwa madhumuni ya kukusanya data kwa mbinu hii ni Misingi ya Fonolojia (2012) na Maendeleo katika Nadharia ya Fonolojia (2011)

**Mbinu ya ushiriki wa mtafiti na Ushuhudiaji**: Mbinu ya ushiriki na ushuhudiaji ulifanyika kwa saa tatu kwa chuo A na saa tatu pia katika chuo B. Somo la fonolojia hufundishwa kwa saa tatu kwa juma, hivyo watafiti walitumia juma moja kwa chuo A na juma moja pia kwa chuo B (kwa nyakati tofauti) kwa kila darasa moja la fonolojia.

Baada ya kukusanywa, data zilizopatikana zilichambuliwa na kisha kuchanganuliwa kwa kutumia mkabala changamano ambapo Mkabala wa Kifafanuzi na Ulinganisho zilitumika.

## UCHAMBUZI NA UWASILISHAJI WA DATA

Makala haya yalilenga kujadili changamoto na mustakabali wa namna ufundishaji wa fonolojia katika ngazi ya Uzamili kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Yafuatayo ni majibu yaliyopatikana kutoka kwa wahadhiri, wanafunzi pamoja na ushuhudiaji.

Kupitia mbinu zote za kukusanyia data, lengo mojawapo ilikuwa ni kufahamu kama kuna matumizi ya uwili lugha (Kiswahili na Kiingereza) katika somo la fonolojia ya Kiswahili. Kupitia ushuhudiaji, katika vyuo vyote viwili na madarasa yote ya fonolojia ya Kiswahili, ilionekana dhahiri kwamba licha ya Kiswahili kubaki kama lugha ya kufundishia na kujifunzia, wahadhiri na wanafunzi hutumia lugha ya Kiingereza katika ufundishaji na ujifunzaji wao. Tofauti iliyobainika miongoni mwa wahadhiri hao ni kiwango cha utumiaji wa uwili lugha kutegemeana na mada na muda anaokuwa darasani kama ni kipindi cha saa moja au kipindi cha saa mbili. Katika Chuo A, katika kipindi cha fonolojia cha saa mbili, mhadhiri alilazimika kutumia istilahi za Kiingereza kuelezea istilahi za Kiswahili, istilahi hizi zilikuwa kumi na mbili katika kipindi kizima. Katika kipindi cha saa moja, mhadhiri alitumia maneno ya saba za Kiingereza zinahusu dhana za kifonolojia. Tofauti ya mhadhiri huyu na wengine ni kwamba yeye, wakati mwingine, alikuwa akitumia Umbo Upeo na fonolojia Mawanda Upeo kutafsiri dhana za kifonolojia alizokwisha kuzisema kwa Kiswahili.

Kwa Chuo B, tofauti na vyuo vingine, katika kipindi cha saa moja, mhadhiri hakutumia kabisa Kiingereza katikati ya kipindi bali alifikia kufanya hivyo alipokuwa akihitimisha kipindi. Wakati huu, mhadhiri huyu alikuwa akitoa kazi kwa wanafunzi wake na kuwaelekeza dhana ambazo walipaswa kuzifanyia kazi. Katika kuzitaja, mhadhiri huyo alikuwa akitaja kwa Kiswahili na Kiingereza. Yaani dhana moja ya fonolojia ilitajwa kwa Kiswahili na Kiingereza. Kwa upande wa kipindi cha saa mbili, hali ilikuwa tofauti zaidi. Darasa hili lilionekana kuathiriwa zaidi na Kiingereza, dhana zilizo nyingi zilionekana kueleweka zaidi zilipoelezwa kwa kuchanganya Kiingereza. Katika darasa hili, ilionekana uwili lugha ni kawaida kwa mhadhiri na wanafunzi wake. Hii ni kwa sababu, wanafunzi wengi walioonekana kushiriki kujibu maswali au kufafanua, hawakumaliza mchango wao bila kuweka kurejea dhana za Kiingereza.

Kupitia mahojiano, wanafunzi wote walidai kuwa wanatumia vitabu vya Kiswahili katika kujifunza au kujisomea fonolojia. Miongoni mwao, wachache walidai hujisomea vitabu vya fonolojia vilivyoandikwa kwa Kiingereza na wengi wao walisema hawasomi vitabu vya Kiingereza na miongoni mwao wengine walidai hawavijui kabisa vitabu hivyo.

Walipoulizwa kama walimu wao hutumia lugha ya Kiingereza katika vipindi vya Kiswahili hususani Fonolojia ya Kiswahili, wote walikubaliana na hilo na kwamba wanapendezwa na matumizi ya uwili lugha katika ufundishaji na ujifunzaji wa fonolojia darasani. Sababu kubwa waliyoitaja ni kwamba wanaelewa kwa urahisi zaidi istilahi au dhana za fonolojia kwa Kiingereza na kwamba istilahi nyingi za kifonolojia hazijaelezwa ipasavyo katika Kiswahili. Pia, walidai kuwa wanapata ugumu katika kujifunza fonolojia kwa Kiswahili kwa sababu wanalazimika kusoma kwa Kiingereza kisha wahawilishe maarifa hayo kwa Kiswahili.

Kwa upande wa wahadhiri, walipoulizwa ikiwa wanatumia Kiswahili wakati wote wa vipindi vya Kiswahili hususani Fonolojia, wote walikataa na kudai kuwa huwa wanalazimika kutumia Kiingereza kwa lengo la kufanikisha malengo ya kipindi. Sababu nyingi walizozitaja hazikuwa

tofauti sana na sababu zilizokwisha kutajwa na watafiti wengine. Miongoni mwa sababu hizo ni kusisitiza jambo au dhana fulani, kumudu darasa, kuhamisha mada ya mazungumzo.

Kwao, tofauti na sababu zilizotajwa katika tafiti zingine, sababu iliyoonekana kubwa zaidi ni kwamba wanakosa msamiati wa Kiswahili kueleza baadhi ya dhana za fonolojia. Hii ni kwa sababu katika Kiingereza, dhana na istilahi za fonolojia zimefafanuliwa vizuri sana na maandiko yake ni mengi na tofauti tofauti ukilinganisha na Kiswahili ambapo vitabu vya fonolojia ni vichache na vilivyopo vimeeleza mambo juu juu na kuna baadhi ya dhana hazieleweki sawa na zilivyozoeleka katika Kiingereza. Kwa mfano, mmoja wao aliuliza istilahi sahihi za Kiswahili zenye kusawiri dhana kama ***"suprasegmental", "autosegmental", "Optimality Theory"*** huku akiuliza maneno yanayotumika kama yanaendana sawa na kinachorejelewa.

Tatizo lingine lililotajwa kuwa linawaletea ugumu kutokana na matumizi ya uwili lugha katika kufundisha fonolojia kwa Kiswahili ni wanafunzi kutokuwa na msingi mzuri wa Kiingereza katika ngazi za chini. Hili huwapa wakati mgumu wahadhiri kulazimika kutafsiri dhana na istilahi za Fonolojia kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili. Waliongeza kuwa kutokana na tatizo la lugha ya Kiingereza kwa wanafunzi wao, wahadhiri hao hujikuta wakitimiza majukumu mara mbili, yaani majukumu yao na wakati huo huo kutimiza ya wanafunzi. Hii ni kwa sababu, kama walivyosema wahadhiri watatu kati ya wanne, wanafunzi wao hugeuka tegemezi na hawajisomei kwa mapana zaidi ya kusubiri kukariri kile kinachokuwa kimetafsiriwa na mwalimu na kuwasilishwa darasani. Waliongeza kuwa ni wanafunzi wachache sana wanaojitahidi kujitafutia maarifa katika vitabu vya Kiingereza.

Kwa hivyo, wahadhiri hao hujikuta wakipoteza muda mwingi kufanya tafsiri badala ya kujikita kwenye jukumu la kuwezesha ujifunzaji. Kadhalika, ilidaiwa kuwa changamoto hii huathiri mbinu za ufundishaji na ushiriki darasani kwa kuwa wanafunzi hubaki wakimtegemea mwalimu na kubakia kuwa watu wa "kutafuniwa na kumeza."[5]

Waaidha, athari nyingine iliyotajwa kuwa inawaletea wahadhiri hao ugumu inatokana na tatizo la istilahi za fonolojia zilizopo katika lugha ya Kiswahili kuwa hazijasawazishwa. Baadhi yao walifafanua kuwa vitabu vya Fonolojia vya Tanzania vinatofautiana katika baadhi ya dhana au ufafanuzi wa istilahi. Kadhalika, vitabu vya mataifa mengine vilivyoandikwa kwa Kiswahili bado, pia, vinatofautiana. Kutokana na changamoto hii, wahadhiri walitaja jukumu za kusawazisha kusahihisha dhana zinazowakanganya wanafunzi wao kama ugumu mwingine wanaokumbana nao na kuwapotezea muda darasani. Pia, msamiati wa Kiswahili katika taaluma za Fonolojia haujasanifishwa ukilinganisha na istilahi zingine.

Jambo lingine lililobainishwa na wahadhiri walioshiriki katika utafiti huu ni tofauti za muhtasari wa fonolojia katika vyuo ngazi za chini. Katika hili, walidai kuwa kutokana na kutokuwepo kwa muhtasari unaofanana katika kiwango cha shule za upili wa juu, astashahada, stashahada na

[5] Kama lilivyotajwa na wahusika.

shahada; wanafunzi wanaojiunga na kiwango cha umahiri wanapata tabu sana kwa sababu baadhi ya istilahi za fonolojia wanakuwa hawazijui na zile wanazozijua zinakuwa zinatofautiana na wakati mwingine zinakuwa si sahihi ukilinganisha na kinacholengwa.

Jambo la mwisho, wahadhiri hao walidai kuwa sababu nyingine inayochangia ni wanafunzi wengi kutokuwa na msingi wa fonolojia katika ngazi za chini. Walioeleza kuhusu jambo hili walidai kuwa hili linasababishwa na mifumo ya baadhi ya vyuo ambapo kozi ya Fonolojia haifundishwi na katika vingine kozi hiyo ni ya hiyari.

**Lengo la pili la utafiti** huu lilikuwa kujua kama vitabu na kazi za wanafunzi za fonolojia ya Kiswahili zimeandikwa kwa Kiswahili fasaha.

Katika sehemu ya lengo hili, watafiti walipitia kazi za wanafunzi watano (5) walizoandika kama kazi za nyumbani kuona namna na kwa kiasi gani zoezi husika limejibiwa kwa kutumia Kiswahili sanifu. Kwa kiasi fulani, wanafunzi walionekana kuandika insha zao kwa Kiswahili sanifu. Pale walipopata ugumu na/ au walipohisi dhana mahususi haielezeki kwa ufasaha walichanganya na lugha ya Kiingereza au walitohoa kutoka lugha ya Kiingereza na kuwa katika lugha ya Kiswahili, kimuundo na kimpangilio wa silabi zake kama inavyojionesha katika sehemu ya majibu kimatini hapa chini:

**a) … kuhusu parameta za…**
**b) …n**adharia **ya gridi…**
c) …uwasilishaji wa **mora** alioupendekeza huundwa …….
**d)** …..katika **gridi**, silabi **nyepesi** … **mora**…
e) **…**uziada Mizani **(Extrametricality**) …
**f) …Kiimbotoni Msingi (Basic Tone Melody)…**

Hapa katika matini haya (a-f), neno *mora, gridi* na *parameta* yametoholewa na dhana za kiimbo toni msingi na uziada mizani yamewekewa pia mbadala wake katika lugha ya Kiingereza. Jambo linalotoa hisia kwamba dhana hizo zinakosa tafsiri bayana katika lugha ya Kiswahili ama inaonekana tafsiri zilizowekwa zinapoteza maana ya dhana ama zinakosa uangavu. Paomoja na mapungufu haya, bado waandishi wa Makala haya, tunaona kwamba wanafunzi wamepiga hatua nzuri katika jitihada ya kukitumia Kiswahili katika kujifunzia fonolojia katika kiwango cha umahiri.

Eneo jingine ambayo watafiti waliangalia matumizi ya uwili lugha katika maandalizi na/au sehemu ya kufundisha ni nukuu za somo ambazo mwalimu anazitumia katika ufundishaji. Katika Chuo Kikuu A, tulipata nafasi ya kuangalia nukuu zilizoandikwa kwa Kinuruweo. Kiujumla, nukuu ziliandikwa katika Kiswahili sanifu isipokuwa katika maeneo machache ambayo mwalimu alisisitiza dhana ama aliona haja ya kuwa na dhana iliyoandikwa katika lugha ya

Kiingereza kwenye mabano kama inavyojionesha katika baadhi ya matini yaliyodondolewa hapa chini:

a) …kuna uwezekano mkubwa wakati wa Mame Bantu ***(Proto−Bantu)*** lugha …

b) … katika lugha ya Kiingereza ni "accent" ikiwa na maana kwamba hubainishwa na kuwepo kwa msikiko wa ziada kwenye silabi inayohusika kuliko silabi nyingine **(relative prominence).**

**c)** …neno husemwa kuwa ina **"accent" au "stress".**

**d)** **…(signifier)** na 'kitajwa', yaani **(signifié)…**

e) … de Saussure alikuja kuiita 'utendaji' (**parole)** na '**lugha' (langue)…**

**f)** …uchanganuzi fulani wa data tuliyopewa ni bora zaidi kuliko uchanganuzi mwingine wowote tunaoweza kupewa **(explanatory adequacy).**

g) … utoshelevu wa uchunguzi **(observational adequacy**).

**h)** …utoshelevu wa maelezo kutokana na jinsi unavyoiona na kuielewa data yako **(descriptive)**

Katika matini (a-h) hapa tunaona kwamba maneno yaliyokolezwa wino yameandikwa kwa lugha ya Kiingereza. Swali la msingi linakuwa ni je lugha ya Kiswahili haijitoshelezi kuzielezea dhana hizo ama tafsiri ya Kiswahili iliyotolewa inaonekana ina uvuguvugu? Hata hivyo bado mwalimu amejitahidi kuandika nukuu ya kozi ya fonolojia kwa lugha ya Kiswahili. Jambo linaloonesha namna Kiswahili kinavyoweza kutumika kufundishia na kujifunzia fonolojia ya Kiswahili.

**Lengo la tatu la utafiti** huu lilikuwa kujua iwapo kuna vitabu vya kutosha vilivyoandikwa kwa Kiswahili vinavyotumika katika kujifunzia na kufundishia kuhusu fonolojia ya Kiswahili.

Katika lengo hili, moja ya nyenzo iliyosaidia kupata mrejesho ni kuangalia vitabu vilivyopendekezwa katika mihtasari kwa kozi ya fonolojia kwa vyuo vyote viwili, chuo A na Chuo B. Katika chuo A, vitabu vilivyopendekezwa kwenye muhtasari ni hivi vifuatavyo:

a) Contini-Morava, E. (1997). "Swahili Phonology" katika *Phonologies of Asia and Africa,* Allan Kaye, Winona Lake, Eisenbrauns (wah)

b) Goldsmith, J.A. (mh) (1996). *The Handbook of Phonology*. Cambridge, Massachusetts: Blackwell Publishers Inc.

c) Halle, M. na G. N. Clements (1983). *Problem Book in Phonology: A workbook for Introductory Courses in Linguistics and in Modern Phonology.* Cambridge Massachusetts: The MIT Press.

d) Hogg, R. na C. B. MacCulley (1987). *Metrical Phonology: A Course Book* Cambridge University Press.

e) Lass, R. (1984). *Phonology: An Introduction to Basic Concepts:* Cambridge, Cambridge University Press.

f) Massamba, D. P. B. (1996). *Phonological Theory: History and Development.* Dar es Salaam: Dar es salaam University Press.

g) Massamba, D. P. B. (2011). *Maendeleo katika Nadharia ya Fonolojia.* Dar es Salaam: Dar es salaam University Press.

h) Massamba, D. P. B. (2012). Misingi ya Fonolojia: Dar es Salaam: Dar es salaam University Press.

i) Mpiranya, F. (1995). *Swahili Phonology Reconsidered in a Diachronical Perspective: the impact of Stress on Morphophonemics and Syllable Structure.* E. A. L. D. Series, Juz. 4. Colobne.

Tunapoangalia kwa makini katika orodha ya marejeo yanayotolewa kwa wanafunzi wa Umahiri

Katika chuo Kikuu A tunaona kwamba kati ya marejeo 9 yaliyotolewa, ni marejeo matatu tu ndio yanaonekana tu yameandikwa kwa lugha ya Kiswahili. Mengine yote yaliyobaki yameandikwa kwa lugha ya Kiingereza. Watafiti walipata nafasi ya kujadiliana kuhusu upatikanaji wa marejeo hayo na kama wanafunzi wanayasoma na kuyaelewa. Wanafunzi watatu (3) tu kati ya (20) walijibu kwamba wanasoma marejeo mengine yaliyoandikwa kwa lugha ya Kiingereza lakini changamoto imekuwa ni vigumu kwao kuelewa dhana kwa kuwa lugha iliyotumika inawatatiza. Hata vitabu vilivyoandikwa kwa Kiswahili upo mchanganyiko ama baadhi ya dhana ,pamoja na kuandikwa kwa Kiswahili lakini yamefafanuliwa kwa kuwekewa katika lugha ya Kiingereza kwa njia ya mabano.

Katika chuo Kikuu B, vitabu vilivyopendekezwa kwenye muhtasari ni hivi vifuatavyo:

a) Archangel, D. and D. Terence. 1997. *Optimality Theory: An overview*. Oxford Blackwell.
b) Hayes, B. 1995. Metrical stress theory: Principles and Case studies. Chicago; University of Chicago Press.
c) Hays, B 2009. Introductory phonology. Oxford: Wiley- Blackwell.
d) Kenstowicz, M. 1994. Phonology in Generative Grammar. Cambridge: Blackwell.
e) Kager, R. Harry van Hulst, and Wim Zonneveld (eds.) 1999. The Prosody- Morphology Interface Cambridge: Cambridge University Press.
f) Massamba, D.P.B 1996. Phonology Theory: History and Development> Dar es salaam: Dar es salaam.

g) Massamba, D.P.B 2005.The role of Suprasegment phenomenon in the Analysis of Bantu of Bantu languages: With special Reference to Ci-Ruuri: in LOT Occasional Papers in Linguistics 1. Dar es salaam.

h) Massamba, D. P. B. (2011). Maendeleo katika Nadharia ya Fonolojia: Dar es Salaam: Dar es salaam University Press.

i) Massamba, D. P. B. (2012). Misingi ya Fonolojia: Dar es Salaam: Dar es salaam University Press.

j) McCarthy, J (ed.). (2004). *Optimality Theory in Phonology.* Victory: Blackwell.
k) Mc Carthy, J. (2008). *Doing Optimality theory: Applying Theory to Data.* Oxford: Blackwell.

Katika chuo B tunaona kwamba kati ya marejeo 11 yaliyotolewa, ni marejeo mawili (02) tu ndio yameandikwa kwa lugha ya Kiswahili. Mengine yote yaliyobaki yameandikwa kwa lugha ya Kiingereza. Watafiti walipata nafasi ya kujadiliana kuhusu upatikanaji wa marejeo hayo na kama wanafunzi wanayasoma na kuyaelewa. Wanafunzi watatu (5) tu kati ya (15) walijibu kwamba wanasoma marejeo mengine yaliyoandikwa kwa lugha ya Kiingereza lakini changamoto imekuwa ni vigumu kwao kuelewa dhana kwa kuwa lugha iliyotumika inawatatiza. Hata vitabu vilivyoandikwa kwa Kiswahili upo mchanganyiko ama baadhi ya dhana ,pamoja na kuandikwa kwa Kiswahili lakini pia, kama ilivyokuwa kwa Chuo A yamefafanuliwa kwa kuwekewa katika lugha ya Kiingereza kwa njia ya mabano.

Picha gani tunaipata kutokana na hali ya marejeo ya namna hii? Zipo hisia mbalimbali zinazoweza kujengwa kutokana na hali hii ya uwepo wa marejeo machache sana yaliyoandikwa kwa lugha ya Kiswahili:

Inawezekana havijaandikwa kwa Kiswahili vitabu vya kutosha vya fonolojia ya Kiswahili

Kuna uwezekano kwamba kuna wataalamu wachache wa fonolojia katika taasisi za elimu ya juu hapa Tanzania ambao wangejishughulisha na utafiti wa fonolojia ya Kiswahili na hatimaye kuiandikwa kwa lugha ya Kiswahili

Fonolojia ya Kiswahili haijatiliwa mkazo katika programu za shahada za awali hasa kwa Chuo Kikuu B, imekuwa kama mada moja wapo katika kozi ya Utangulizi wa Isimu kwa ujumla. Hivyo mada za fonolojia ya Kiswahili zimefichama kwatika mwamvuli wa isimu kwa ujumla.

Kwa upande wa wanafunzi, kuna madhara ya hali ya kuwa na marejeo mengi yaliyoandikwa kwa lugha ya Kiingereza ni kwamba mwanafunzi hulazimika kutumia muda mwingi kusoma ili ahamishe dhana hizo katika lugha ya Kiswahili, hivyo kumpotezea muda. Baadhi ya dhana za

msingi katika mada mahususi huenda zisieleweke au kutafsiriwa ipasavyo, hivyo kurudisha ari ya kusoma fonolojia ya Kiswahili au kuonekana kama kozi ngumu yenye udhahania uliopitiliza.

Kwa upande wa wafundishaji, hupata ugumu wa ufundishaji hasa kulazimika kufanya tafsiri ya dhana zilizopo katika lugha ya Kiingereza na kuziakisi katika lugha ya Kiswahili, hivyo ufundishaji kuchukua taswira kana kwamba ni somo la tafsiri wakati ni somo la fonolojia ya Kiswahili. Hali hii ilijionesha kwenye Chuo B, Zaidi ambapo marejeo ya msingi yaliyo kwenye lugha ya Kiingereza ilionekana imetafsiriwa kwenye *powerpoint*. Hali hii pia humchosha mwalimu kufanya majukumu zaidi ya ufundishaji na kufanya tafsiri zaidi.

## HITIMISHO

Kulingana na data zilizopatikana kupitia mbinu ya ushuhudiaji na ile ya mahojiano. Tunahitimisha kwamba wahadhiri na wanafunzi wa kozi za Fonolojia katika ngazi ya Uzamili hutumia uwili lugha kwa kiasi kikubwa. Ingawa Kiswahili hubaki kama lugha kuu ya mawasiliano, kufundishia na kujifunzia katika vipindi vya kozi hiyo, Kiingereza pia hutumika wakati wa ujifunzaji ndani na nje ya darasa na hutumiwa na washiriki wote (wahadhiri na wanafunzi).

Tofauti na sababu zingine za uwili lugha zilizozoeleka, matumizi ya uwili lugha (Kiswahili na Kiingereza) katika ufundishaji wa kozi hii hayachangiwi na sababu za kimawasiliano kwa kiasi kikubwa bali changamoto lukuki zinazoikumba kozi hiyo katika ngazi ya umahiri. Hii ni kusema kwamba wahadhiri na wanafunzi wa kozi ya Fonolojia katika ngazi ya Uzamili wanalazimika kutumia mtindo wa uwili lugha ili kufanikisha uelewa na malengo ya kozi hiyo. Changamoto kubwa zinazopelekea mtindo huu ni uhaba wa matini za fonolojia zilizoandikwa kwa Kiswahili, matini za fonolojia zilizoandikwa kwa Kiswahili hazifanani si katika kiwango cha kitaifa wala kimataifa. Changamoto nyingine ni kwamba istilahi na dhana nyingi za fonolojia hazijafanyiwa tafsiri. Kadhalika, wanafunzi wanaojiunga katika programu hii (Uzamili) wanakuwa hawana msingi mzuri wa Fonolojia kwa kuwa hakuna muhtasari unaofanana katika vyuo.

Kutokana na matumizi ya uwili lugha, athari mbalimbali zinaukumba mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji wa Fonolojia katika kiwango cha Uzamili. Athari kubwa zaidi ni kwamba uwili lugha kukwamisha uelewa kwa wanafunzi na kupoteza muda kwa kuwa wahadhiri na wanafunzi hujikuta wakiishia kufanya tafsiri badala ya kujikita kwenye kufafanua istilahi na dhana za fonolojia. Hii ni kwa kuwa kupitia mbinu hii watu hao hujikuta wakilazimika kupitia hatua tatu zaidi. Mosi, kusoma matini za Kiingereza na kuzielewa. Pili, kuhawilisha maarifa waliyoyapata kutoka Kiingereza kwenda kwenye Kiswahili. Tatu, kuhakikisha msamiati uliotumika kueleza maarifa hayo kwa Kiswahili ni sanifu. Jambo hili hupoteza muda na kukwamisha upataji maarifa kwa haraka na pia huleta mkanganyiko na mwisho hupelekea wanafunzi kukariri dhana na istilahi badala ya kuelewa. Athari zingine ni kuathiri mbinu za ufundishaji, kukwamisha malengo ya kozi au wahadhiri, pamoja na kutilia maanani maarifa

yanayoegemea katika ujenzi wa kumbukumbu badala ya ujuzi kama inavyokusudiwa katika kiwango cha umahiri.

Kwa ujumla, pamoja na changamoto za tafsiri na ukosefu wa vitabu vya rejea vilivyoandikwa kwa lugha ya Kiswahili, upo mwanga mkubwa kwamba lugha ya Kiswahili inaweza kutoa maarifa ya kutosha kuhusu taaluma ya fonolojia kwa ujumla wake. Hata hivyo, bado ipo haja kusaidia kuona namna ambavyo maboresho yanaweza kufanyika hasa katika kipengele cha tafsiri za istilahi za fonolojia yanavyoweza kusaidia kukuza taaluma ya fonolojia na lugha ya Kiswahili kwa ujumla kwa kuwa vitabu mbalimbali vya fonolojia (vingi) vimeandikwa kwa lugha ya Kiingereza ambayo huwatatiza wajifunzaji na wafundishaji.

**Mapendekezo**

Kulingana na data zilizopatikana na mjadala katika makala haya, utafiti huu unapendekeza yafuatayo.

- Kuhamasisha zaidi wataalamu wa Fonolojia kuandika vitabu vya fonolojia kwa Kiswahili vingi na vyenye ubora zaidi katika taaluma hiyo.
- Kuandikwa kwa kamusi ya istilahi za taaluma za Fonolojia.
- Kuhamasisha wanafunzi wa umahiri kusoma vitabu vilivyoandikwa kwa Kiingereza ili kupanua maarifa yao.
- Somo la Fonolojia lifanywe kama somo la lazima kwa vyuo vyote vinavyotoa kozi zinazohusiana na isimu ya lugha.
- Kuwepo kwa muhtasari wa fonolojia ya Kiswahili uliosawazishwa kwa vyuo vyote ili kuepusha changamoto za sasa.
- Somo la Fonolojia lifundishwe ipasavyo kuanzia ngazi za chini ili kuwajengea wanafunzi msingi mzuri kwa ngazi zinazofuata.

**MAREJELEO**

Bhatti, A., Shamsudin, S. na Said, S. B. M. (2018). Code-Switching: A Useful Foreign Language Teaching Tool in EFL Classrooms. *English Language Teaching,* 11(6), 93-101.

Brisk, M. E. (2000). Education Quality Bilingual Defining Success. *LAB Working Paper No. 1*

Brown, G. na Atkins, M. (1988). *Effective Teaching in Higher Education.* London na New York: Routledge.

Contini-Morava, E. (1997). “Swahili Phonology” katika *Phonologies of Asia and Africa,* Allan Kaye, Winona Lake, Eisenbrauns (wah)

Du Plessis, T. (2006). From Monolingual to Bilingual Higher Education: The Repositioning of Historically Afrikaans-Medium Universities in South Africa. *Language Policy,* 5(2006), 87-113.

Flyman-Mattsson, A. na Burenhult, N.(1999). Code Switching in Second Language Teaching of French. Lund University, Dept. of Linguistics. *Working Papers,* 47 (1999), 59-72

García, O., na Wei, L. (2014). *Trans-languaging: Language, bilingualism and education*. Basingstoke: Palgrave Macmillan.

Goldsmith, J.A. (mh) (1996). *The Handbook of Phonology*. Cambridge, Massachusetts: Blackwell Publishers Inc.

Halle, M. na G. N. Clements, (1983). *Problem Book in Phonology: A workbook for Introductory Courses in Linguistics and in Modern Phonology.* Cambridge Massachusetts: The MIT Press.

Hogg, R. na C. B. MacCulley, (1987). *Metrical Phonology: A Course Book* Cambridge University Press.

Ibrahim, E. H. E., Shah, M. I. A. na Armia, N. T. (2013). Code-Switching in English as a Foreign Language Classroom: Teachers' Attitudes. *English Language Teaching*, 6(7),139-150.

JMT. (2014). *Sera ya Elimu na Mafunzo.* Dar es Salaam: Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Johanes, J. (2017). *The Influence of Code-Switching and Code-Mixing on Learning English Language in Secondary Schools: The Case of Rombo District.* Utafiti usiochapishwa.

Langner, M. na Imbach, R. (2000). The University of Freiburg: A Model for a Bilingual University. *Higher Education in Europe*, 25(4), 461- 468.

Lass, R. (1984). *Phonology: An Introduction to Basic Concepts:* Cambridge, Cambridge University Press.

Lewis, C. L. (2008). *Teachers' Knowledge of English Phonology and Attitudes toward Reading Instruction as Related to Student Outcomes.* Utafiti Usiochapishwa.

Lin, A. M. Y. (2013). Classroom Code-switching: Three Decades of Research. *Applied Linguistics Review*, 4(1): 195-218.

Madrid, D. and Julius, S. M. (2017). *Quality Factors in Bilingual Education at the University Level.* Haijachapishwa.

Makulloluwa, E. (2013). Code Switching by Teachers in the Second Language Classroom. *International Journal of Arts & Sciences, 6(3):581–598.*

Marie, K. A. (2013). Coping with English as Language of Instruction in Higher Education in Rwanda. *International Journal of Higher Education,* 2(2), 1-12.

Massamba, D. P. B. (1996). *Phonological Theory: History and Development.* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Mpiranya, F. (1995). *Swahili Phonology Reconsidered in a Diachronical Perspective: the impact of Stress on Morphophonemics and Syllable Structure.* E. A. L. D. Series, Juz. 4. Colobne.

Rugemalira, J. (2017). *Language Skills for Higher Education in Tanzania.* Haijachapishwa.

Shartiely, N. E. (2016). Code-switching in university classroom interaction: A Case Study of the University of Dar es Salaam. *Stellenbosch Papers in Linguistics Plus,* 49(2016), 215-231.

Songxaba, S. L., Coetzer, A. na Molepo, J. M. (2017). Perceptions of Teachers on Creating Space for Code Switching as a Teaching Strategy in Second Language Teaching in the Eastern Cape province, South Africa. *Reading & Writing* 8(1), 1-7

Villarreal, A. na Solís, A. (1998*). Effective Implementation of Bilingual Programs: Reflection from the Field.* Haijachapishwa.